



Wakuu wa Idara na Vitengo wa
kiwa katika picha ya pamoja na Wakurugeni na Mwenyekiti wa
Halmashauri baada ya makabidhiano



Mwenyekiti wa Halmashauri akiwa ktika picha ya pamoja na
Wakurugenzi Melkzedek Humbe kushoto na Charles Fussi kulia



Wakurugenzi Melkzedek Humbe na Charles Fussi katika picha ya pamoja baada ya makabidhiano ya ofisi



Mkurugenzi Charles Fussi akiwa amembatana na afisa kilimo Fadhili Chimsala na Mbaguzi wa ndani Mr Rweikiza wakimuonyesha mashamba ya korosho Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Halmashauri ya Manyoni Bw Melkzedek Humbe



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Mh Jumanne Mlagaza akitoa shukrani kwa aliyekuwa mkurugenzi wa Halmashauri Charles Fussi kwa kuweza kukabidhi ofisi kwa Mkurugenzi anayechukua nafasi yake

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Melkzedeki Humbe akabidhiwa ofis



Posted on: august 15th,2021

Makabidhiano ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni yamefanyika tarehe 14 agosti 2021. Bw Melkzedek Humbe ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji mteule wa Halmashauri Wilaya ya Manyoni amekabidhiwa Ofisi na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Bwa Charles fussi.

Katika makabidhiano hayo Bw Melkzedek amesema kuwa anategemea ushirikiano mkubwa kutoka kwa Viongozi wa Wilaya na wakuu wa vitengo na Idara na watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Amesisitiza kwamba bila ushirikiano hakuna kitakachoweza kufanyika .Humbe ametoa pongezi kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manyoni Bw Charles Fussi kwa kipindi chote alichoweza kuhudumu kama Mkurugenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na kwa hatua kubwa ya usimamimizi na ubunifu mradi wa kilimo cha korosho.

Aidha Humbe aliongeza kuwa yeye hajaja kuanzisha kazi bali kuendeleza kazi iliyoachwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halimashauri Charles Fussi na kwamba kama ambavyo kauli ya mama Samia Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania isemavyo kwamba kazi iendelee basi n a ndivyo anavyotamani Manyoni iendelee kazi alizokuwa akifanya Fuss ziendelee.

“Mimi sijaja kuanzisha kazi upya bali nimekuja kuendeleza yale ambayo mwenzangu aliweza kuyaibua lakini yaliyo ya utekelezaji wa ilani pia maendeleo ili kuleta tija kwa hivyo naomba niseme kazi iendelee na si kazi ianze” alisema Humbe.

Kwa upande wake aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Bw Charles Fussi amewashukuru watumishi wote na kuahidi kwamba ataendelea kutoa ushirikiano pale watakapoona inafaa ili kuleta tija ya maendeleo kwa wananchi wa Wilaya ya Manyoni.

Aidha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ametoa shukrani kwa Bw Fussi kwa kipindi chote walichoweza kufanya kazi pamoja na amesema kuwa anaamini kwamba Mkurugenzi aliyekabidhiwa Ofisi ataendeleza ushirikiano wa utendaji kazi kati ya Ofisi ya Mkurugenzi na ofisi yake.

Makabidhiano hayo yamehudhuriwa na Wakuu wa Idara na Vitengo vyoe na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. na baada ya makabidhiano ya ofisini ya nyaraka basi waliweza pia kutembelea mradi mama wa kilimo cha korosho katika maeneo yote yalipo mashamba hayo .